# MWONGOZO PP2

**Karatasi ya 2:102/2 Lugha**

**1. Ufahamu**

**(a)**Tambua sifa tatu hasi za Athumani. (alama 3)

**mwenye kiburi**

**mwenye madaha**

**mwenye kujitakia makuu**

**(b)**Thibitisha kuwa Athumani ni *msiri*

**alipanga mambo yake kisiri**

**(ch)** Onesha changamoto za safari za mabasi kulingana na kifungu. *(alama 3)*

**kuvamiwa na majambazi**

**kusimamasimama ili abiria wajisaidie**

**kero nyingi kutoka kwa baadhi ya wasafiri**

(d) Jadili mafunzo aliliyopata Athumani. (alama 2)

**kutofanya mambo kisiri**

**kutokula vyakula kiholela njiani**

(e) Kwa nini Athumani alikataa mtu yeyote kujua kwamba anaenda kufanya mahojiano? (alama 1)

**kazi hiyo ilikuwa na donge nono**

(f) Jadili sifa mbili za dereva (alama 2)

**mwenye makini**

**mwenye utu**

(g) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i) gugumia. ii) ng'oa nanga iii) himili.

**meza kwa nguvu,anza safari,vumilia**

**2. Ufupisho**

(Alan

**(a)** Eleza madhara ya sukari kwa maneno kwa maneno 120

**Ni** sumu mwilini. husababisha maisha mafupi,haina virutubishi,Ina asidi nyingi,meno kuharibika,meno kuuma,maradhi ya kisukari,kichefuchefu,matatizo ya kuona,maradhi ya ngozi na figo, ongezeko la kolestroli na moyo kuchoka

(Ala

**(b)** Eleza manufaa ya sukari ya asali kwa maneno kwa maneno 70

huupa mwili vitamini, madini na amino asidi. Pili, sukari ya asali huupa mwili nishati. Huchangamsha mwili,watoto kukua vizuri, husaidia usagaji wa chakula, husaidia mwili kujikinga na maradhi kama homa, huzidisha kiwango cha himoglobini na kupunguza uwezekano wa watoto wadogo kupata anemia. huondoa harufa mbaya kinywani,hufanya ngozi kung'ara, huondoa vipele na ugumu wa ngozi, hutibu kule ngozi imekatikakatika na vidonda vilivyotokana na kuchomeka.

C; Matumizi ya lugha

**(Alama 40)**

**3. Matumizi ya lugha**

**Jibu maswali yote yafuatayo.**

**a) Andika sauti moja sighuna ambayo ni kikwamizo cha ufizi.** **(alama1)**

/s/

**b) Andika neno lenye muundo wa silabi ya irabu tatu pekee.** **(alama1)**

, aua, aoa, aoe, aue, eua, iue, uue.

c) Jadili sifa mbili za kimadende zinazohusisha ulimi (alama 2)

Ncha ya ulimi hupigapiga kaakaa gumu

Hupigapiga kwa kasi

**d) Eleza maana ya sauti mwambatano kisha utoe mfano ya itamkiwayo ufizini** **(alama2)**

Konsonanti mbili au zaidi ambazo hutamkwa kama sauti moja au sauti mbili au zaidi zinazotamkw kama sauti moja ndoa /nd/ /tw/ /nz/ /ndw/ /nw/ ndwele, ndama

**e) Andika sauti zenye sifa zifuatazo** **( alama 2)**

i) **Nazali ya kaakaa laini**
ii) **Kikwamizo ghuna cha mdomo na meno**
iii) **Irabu ya nyuma wastani**
iv) **Kiyeyusho cha kaakaa gumu**
i) /ng'/
ii) /v/
iii) /o/
iv) /y/

**Akifisha sentensi hii ili kuleta maana mbili tofauti kwa kurejelea kiimbo. Jirani yangu amewasili** **(alama2)**

Jirani yangu amewasili. (taarifa au kauli)

Jirani yangu amewasili? (swali)

Jirani yangu amewasili! (mshangao)

f) **Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno** **(alama2)**

Sehemu ya neno inayobeba maana ya kimsingi/haibadiliki hata ukiambishwa/kunyambuli
Huweza kuwa na maana, kamili kama sahau, amini
Inayobeba wazo kuu
Isiyoweza kuleta maana mpaka iambishiwe
Itumikiayo kuunda maneno mengine.

g) **Andika neno moja lenye mofimu zifuatazo:**
**Nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa wingi, mzizi wa kitenzi imba, kaul tendesha, kauli tenda** **(alama 2)**
Tuliwaimbisha

h) Onyesha matumizi ya kiambishi **na** kama kiambatanishi (alama 2)

Mama alienda <u>naye</u> shambani

i) **Eleza matumizi ya kiambishi 'ki'katika sentensi hii.** **(alama2)**
**Njia hii haipitiki**
<u>Kutowezekana</u> kwa kitu fulani

**Kiambishi- U-hutambulisha majina yote ya ngeli ya U (umoja). Hata hivyo baadhi maji haya huchukua viambishi tofauti tofauti katika wingi. Orodhesha majina ma kama hay kisha uonyeshe viambilshi hivyo tofauti vya ngeli (Katika umoja na Wingi)**
**(alama2)**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| u | ny | mf | uzi-nyuzi | uta-nyuta |
| u | k | mf | ukuta – kuta | ukope- kope |

| | | | |
|---|---|---|---|
| u | m | mf | ugonjwa – magonjwa |
| u | f | mf | ufagio- fagio |
| u | mb | mf | ubao – mbao |
| u | nd | mf | ulimi- ndimi |
| umoja | | mf | waraka- nyakara / wayo- nyayo |

j) **Kanusha sentensi hii.** **(alama 2)**

**Kila achezapo Kaissa, huumiza mkono wake**

Kila asipocheza Weloba haumizi mkono wake. *au*

Kila asipocheza Weloba huwa haumizi mkono wake.

k) **Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari**

**Ubora wa kazi zao ulifichika baada ya kuanzishwa kwa mradi ule.**

Ubovu /uduni wa kazi zao ulifichuka kabla ya kumalizwa kwa mradi ule *alama 3*

l) **Tofautisha vitate hivi, tuni na duni kisentensi** **alama 2**

Tuni –sauti ya ala au wimbo Duni –hafifu

m) **Ndovu wa Kiafrika ameharibu kichaka** **(alama 2)**

Jidovu la kiafrika limeharibu jichaka au

Ndovu la kiafrika limeharibu chaka

n) **Tumia nomino ya jamii kuwakilisha maneno yaliyopigiwa mstari.** **(alama1)**

o) **Nzige wengi sana walivamia na kuharibu mimea.**

Wingu la nzige au jeshi la nzige

**Yaandike maneno yafuatayo katika ufupi wake**

**Shangazi zako**

**Mama zako** **(alama 2)**

Shangazizo

Mamazo

**p) Tunga sentensi kubainisha matumizi ya** **(alama 2)**

**–enye-** Sanduku lenye fedha limeibwa. (kuonyesha umiliki)

**-enyewe-** Sanduku lenyewe limepatikana.(kuonyesha msisitizo au kutilia mkazo)

**r) Tunga sentensi yenye muundo ufuataao:** **(alama2)**

**KN (N) + KT (T + E) + U + KN (N) + KT (T + E)**

Njuguna huandika vyema lakini Zuhura huandika vibaya.

**s) Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii** **(alama2)**

Nomino dhahania – upendo/urembo/chungu/wima/wivu nk

Nomino – jamii, umati, askari, halaiki
Sentensi moja pekee – nomino dhahania + ya jamii.
Upendo wa askari unamtia.

t) **Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mistari** **(alama 1)**

**<u>Mtalii</u> atazuru <u>mbuga</u>**

<u>Yeye atazuru kule</u>

<u>u)</u> **Andika sentensi ifuatayo katika umoja.** **(alama 2)**

**Hao wenyewe hawakuzingatia mafunzo ya lishe bora.**

Huyo mwenyewe hakuzingatia funzo la lishe bora.

v) **Andika kwa ukubwa wingi.** **(alama2)**

**Nyoka hatari wamepanda mtini.**

Majoka hatari yamepanda majitini.

w) **Fafanua maana za misemo ifuatayo kwa kuitungia sentensi**

**Kula uyundo-** kutofaidika, kupata hasara, kupata shida, kula mwata. **( alama 2)**

**Kula uhondo** - kupata starehe/neema/raha/ufanisi/manufaa/faida/utamu

x) **Akifisha:**

**Sijaona kitabu kizuri kama hiki utaniazima siku ngapi bashiri alimuliza sijaona.(ala. 4)**

"Sijaona kitabu kizuri kama hiki, utaniazima siku ngapi?" Bashiri alimuuliza sijaona au

Sijaona, Sijaona kitabu kizuri kama hiki, utaniazima siku ngapi? Bashiri alimuuliza Sijaona

Au

Bashiri alimwuliza Sijaona, "Sijaona kitabu kizuri kama hiki, utaniazima siku ngapi?

Isimu jamii

**Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanovyodhibiti mitindo ya lugha.**

**Mazingira** **(alama 4)**

Mzungumzaji huchota msamiati kutoka mahali kutoka mahali anapozungumza kama soko na mahakama.
Mazingira huathiri kiimbo/shadda/Tòni
Huathiri uteuzi wa lugha/lahaja k.m mazingira rasmi huhifadhi lugha rasmi.
Hudhibiti kiwango cha usanifu au urasmi wa lugha k.m mazingira yasiyo rasmi hayahitaji kutumia lugha yenye rasmi/sanifu.
Hudhibiti mtindo nafsi wa mtu k.m biashara ya rejareja- kuna kujirudiarudia.
Hudhibiti ishara anazotumia mtu. Zipo ishara za uso au miondoko ambazo hazikubaliki kulingana na tamaduni /mazingira fulani.

**Madhumuni** **(alama 2)**

Lengo la mawasiliano huathiri jinsi mtu anayotumia lugha k.m unapoonya huwa mkali.
Huathiri shadda/kiimbo – kama madhumuni kusisitiza, kiimbo cha juu hutumiwa.

**Malezi** **(alama 4)**

Mtoto aliyelelewa kwa kudhibitiwa huinukia kutoweza au kutomudu/kujieleza vyema kwa sababu ya uoga aliojazwa
Mtoto anayelelewa katika mazingira ya unyanyasaji hutumia lugha kali ya kujihami.
Akielelewa na wazazi wanaozungumza lugha mbili au zaidi huweza kujifunza/kutumia zote mbili
Mtoto aliyelelewa akihimizwa kujieleza huinukia kuwa na uwezo ukakamavu wa kujieleza.
Mtoto asipofunza lugha mama hushindwa kujieleza kwa lugha hiyo.
Mtoto hufunzwa kuepuka matumizi ya msamiati au lugha ya aibu au kali.
Akilelewa katika matumizi ya lugha ya juu – pia yeye ataitumia.
Msamiati mchafu- mtoto naye atakuwa vivyo hivyo.